

**ENVIRONMENTAL AND SOCIAL IMPACT ASSESSMENT REPORT
FOR THE CONSTRUCTION OF FAECAL SLUDGE TREATMENT
PLANT IN MAGU TOWN, MAGU DISTRICT, MWANZA REGION
(LVWATSAN –MWANZA)**

**Non – Technical Executive Summary
(English and Swahili Version)**

PREPARED FOR:

Mwanza Urban Water and Sanitation Authority (MWAUWASA) /
European Investment Bank (EIB)
P.O. Box 317
Makongoro Road, Mwanza

PREPARED BY:

Mott MacDonald in association with UWP Consulting
& Mr. Ally Salim (Registered Environmental Expert)
P.O. Box 175
Sengerema, Mwanza – Tanzania
Tel.: +255 754 432 400, +255 784 998 202
Email: ally.salim@gmail.com

SUBMITTED TO:

NEMC Lake Zone
P.O. Box 11045
Maji Igogo, Mwanza – Tanzania
Tel.: 0282502684
Email: nemcmza@gmail.com



19th, September, 2016

EXECUTIVE SUMMARY

A: Title and Location of the Project: Proposed Construction of a Faecal sludge treatment plant in Magu town, Magu District, Mwanza region

B: Name and Contact of the Proponent:

Mwanza Urban Water and Sanitation Authority (MWAUWASA) /
European Investment Bank (EIB)
P.O. Box 317
Makongoro Road, Mwanza

C: Name and Contacts of consultants undertaking this ESIA study:

Mott MacDonald in association with UWP Consulting &
Mr. Ally Salim (Registered Environmental Expert)
P.O. Box 175
Sengerema - Mwanza – Tanzania
Tel.: +255 754 432 400, +255 784 998 202
Email: ally.salim@gmail.com

A Brief Outline and Justification of the Proposed Project

The *Lake Victoria Water and Sanitation (LWATSAN) – Mwanza Project*, funded by the Ministry of Water and Irrigation (MoWI) and the European Investment Bank (EIB), and implemented between 2014 and 2019, aims at protecting the Lake Victoria environment and wellbeing of the population in the Lake Basin. The Project has several components, one of these being the construction of a faecal sludge treatment plant for Magu town.

The overall layout is designed for a total of four settling-thickening ponds with two drying beds for each pond. Only the first two units (Ponds A and B) will be constructed initially with space reserved for future expansion for additional capacity (Ponds C and D).

The project will be located at 5 kilometers from Mwanza – Musoma tarmac road; currently the site is used for rice plantation with few acacia plant species. No people nearby the proposed development. The area is in below compared with Magu Town with a different of 5 meters above the sea level.

An Environmental and Social Impact Assessment (ESIA) study for these works for Magu town was conducted in January-August 2016; the results have been presented in an ESIA report that was completed on 19 August 2016, and then submitted to NEMC for review and approval.

In Magu town there is no established faecal sludge treatment for the waste being generated in septic tanks and pit latrines. The local administration organizes private operators with suction trucks to empty septic tanks and latrines and when a minimum number of users are willing to pay, the private operator is called to service several sites at the same time. As there is no appropriate site for disposal of the faecal sludge waste, the waste is dumped in the fields nearby where the private operator has an agreement with the landowner. The works focus on developing a disposal facility near Magu to reduce transportation costs and provide hygienic treatment of the faecal sludge. Construction works, to be implemented simultaneously with water supply works (being subject of a separate ESIA) are expected to start in November 2016, to last for 24 months, followed by a defect period of 12 months.

The land selected for the disposal site is government-owned property by the Magu District Council after paying compensation to the local people who initially owned it. Expected negative impacts of construction of the works require the usual set of mitigation measures associated with this sort of work: prevention of soil erosion due to excavation works, pollution of soil and water, noise and dust, spreading of disease, and assuring safety for workers and the general public at construction sites. Operation of the site has been designed to minimize the risk of contamination of the environment through the separation of solids and liquids using settling-thickening ponds, from where each fraction is treated and disposed off separately.

Potential concerns for groundwater protection are pathogen movement in the groundwater and the infiltration of soluble nutrients. Due to their size, the pathogens will adhere to the soil particles and not move far. Soluble nutrients, such as nitrate from urine, will move with the groundwater, but will be diluted to a level where there is no health risk. It is assumed that most of the nitrate has already infiltrated at the site of origin, that is near the households from the infiltration of liquid waste the septic tanks and pit latrines. For re-use of the dried faecal sludge, the operation will secure elimination of *Ascaris* eggs by allowing a three years retention time before final removal of the material.

It is therefore concluded that the negative impacts associated with the proposed intervention are generally site-specific, short-term, reversible in nature, low significance, and can be easily mitigated and that major adverse impacts of the planned interventions are not expected. The usual package of mitigation measures associated with this sort of development are recommended to prevent soil erosion due to excavation and back-filling works, pollution of soil and water sources, dust and noise, spreading of disease and assuring safety for workers and the public in general. A systematic assessment of expected impacts of the intervention learns that the planned development is expected to lead to improved health and sanitation for the population of Magu town.

**TATHIMINI YA ATHARI YA MAZINGIRA NA KIJAMII YA MRADI
WA UJENZI WA DAMPO LA KUTIBIA MAJI TAKA KATIKA MJI WA
MAGU, WILAYA YA MAGU, MKOANI MWANZA**

(Muhtasari Rasmi usio wa Kiufundi)

MWENYE MRADI:

Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) /
Benki ya Maendeleo ya Ulaya (EIB)
S. L.P 317
Barabara ya Makongoro, Mwanza

MWANDAAJI WA TAARIFA:

Washauri Waelekezi: Mott MacDonald pamoja
na UWP kwa kushirikana na Ally Salim
(Mshauri Mwelekezi wa Mazingira)
S. L. P. 175
Sengerema, Mwanza – Tanzania
Simu +255 754 432 400, +255 784 998 202
Barua Pepe: ally.salim@gmail.com

INAKOWASILISHWA:

Baraza la Taifa la Uhifadhi na
Usimamizi wa Mazingira
Ofisi ya Kanda ya Ziwa
S. L.P 11045
Maji Igogo, Mwanza – Tanzania
Simu: 0282502684
Baruapepe: nemcmza@gmail.com



19, Septemba, 2016

MAELEZO YA MRADI KWA UFUPI

Mradi wa Maji Safi na Maji Taka katika Mkoa wa Mwanza unafadhiliwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Ulaya, ambao utekelezaji wa mradi huu ni katika kipindi cha 2014 na 2019, lengo kuu likiwa na kulinda Mazingira ya Ziwa Victoria na uhai wa watu wanaoishi katika eneo la Bonde la Ziwa Victoria.

Mradi huu unahusisha ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya maji safi pamoja na maji taka, miongoni mwa miradi itakayotelezwa katika mradi huu ni pamoja na ujenzi wa dampo kwa ajili ya kutibia maji taka katika mji wa Magu.

Mradi huu wa ujenzi wa dampo la maji taka utahusisha ujenzi wa mabwawa manne yenye pande mbili za kuchujia kwa kila moja, ingawa katika awamu hii ya kwanza ya mradi itahusisha ujenzi wa mabwawa mawili ambapo eneo litakalobakia litakua kwa ajili ya upanuzi wa ujenzi wa bwawa la tatu na la nne.

Eneo la mradi litakua umbali wa kilometre 5 kutoka barabara ya Mwanza- Musoma, eneo hilo kwa sasa linatumia kwa kilimo cha mpunga pia lina miti michache ya jamii ya *Akashia*, ingawa hakuna makazi karibu. Pia uchaguzi wa eneo hilo umezingatia mwinuko toka usawa wa bahari ambao ni tofauti ya mita za mwinuko 5 kulinganisha na mwinuko wa Mji wa Magu, hii ni kwa kuangalia endapo kama kutakuja kuwa na mfumo wa maji taka wa mabomba, maji taka yataweza kumiminika kwa gravity (bila kusukumwa kwa pampu)

Kulingana na Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005, miradi hii inahitaji kufanyiwa tathmini ya athari ya mazingira na kijamii, ambapo kwa mradi wa Maji taka mjini Magu tathmini ilifanyika katika kipindi cha kuanzia Januari – Agosti 2016, na majibu ya tathmini hii yalikamilika 19 Agosti 2016 na kuwasilishwa katika Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, Ofisi ya Kanda ya Ziwa kwa ajili ya uhakiki na kupitishwa

Katika Mji wa Magu kwa sasa hakuna dampo maalumu kwa ajili ya kumwaga na kutibia maji taka yanayozalishwa na kuhifadhiwa katika mashimo ya maji taka na mashimo ya vyoo. Kwa hivyo utaratibu umekuwa wa kutumia watu binafsi au makampuni yenye magari yanayobeba maji taka kwa ajili ya kunyonya maji taka pindi kunapokuwa na wananchi wanaohitaji kupata huduma hiyo na ambao wapo tayari kulipia gharama za kunyonyewa maji taka. Ingawa

hakuna eneo maalumu kwa ajili ya kumwaga maji taka, mwenye gari la maji taka kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Magu wanatumia maeneo ya wazi baada ya kufanyika makubaliano na mwenye eneo kwa ajili ya kumwaga maji taka hayo.

Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kujengwa karibu na mji na Magu mjini ili kupunguza gharama za usafirishaji na kuimarisha usafi katika kutibu maji taka. Ujenzi wa mradi utakua unajengwa kwa kippindi kimoja na ujenzi wa mradi wa maji safi katika Mji wa Magu ambao unatarajiwa kuanza ujenzi wake katika kipindi cha Novemba 2016 na kukamilika katika kipindi cha miezi 24, kikifuatiwa na kipindi cha majaribio cha miezi 12

Eneo la mradi tarajiwa wa maji taka linamilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Magu baada ya kulipa fidia kwa wananchi waliokuwa wanamiliki eneo hilo kufuata sheria na taratibu za nchi.

Athari hasi zinazotarajiwa kujitokeza kutokana na ujenzi huu zitahitaji kuchukuliwa hatua mbadala kwa ajili ya kupata ufumbuzi wa athari hizo. Miongoni mwa hatua mbadala ni pamoja na kuzuia mmomonyoko wa ardhi unaosababishwa na uchimbaji na ufukiaji wa ardhi, uchafuzi wa maji na udongo, makelele na vumbi, kuenea kwa magonjwa, pamoja na kuhakikisha afya na usalama wa wafanyakazi na jamii kwa ujumla katika maeneo ya ujenzi.

Uendeshaaji wa mradi huu umebuniwa katika namna bora ya kupunguza madhara ya kimazingira kwa kutenganisha taka ngumu na taka maji kwa kutumia mfumo wa mabwawa ambayo kila moja litatibiwa na kuteketezwa kipekee bila kuwa na madhara. Kuhusiana na utunzaji wa maji ya ardhini, jambo kubwa ni kusambaa kwa wadudu / vimelea na kujichuja na kuingia katika mikondo ya maji. Kulingana na ukubwa na ubunifu wa mradi, wadudu / vimelea vitasambaa katika udongo na havitasambaa kwa umbali mrefu.

Mchanganyiko wa vimelea, kama wadudu wapatikanao kwenye mikojo, watatembea pamoja na maji ya ardhini, ingawaje maji taka yatatibiwa katika kiwango ambacho wadudu hao watakosa nguvu za kuendelea kuishi. Vimelea vingi vinatarajiwa kunyonywa katika maeneo ya uzalishaji wa maji taka, karibu na maeneo ya jirani na nyumba ambako ndiko vyanzo vya maji taka viliko kama vile mashimo ya maji taka na mashimo ya vyoo.

Mabaki ya maji taka ambayo yakakuwa katika mfumo wa taka ngumu yatahifadhiwa kwa kipindi cha miaka mitatu kwa ajili ya kuivishwa kwa kuondoa wadudu na mayai ya wadudu na baada ya hapo yatatumiwa na wakulima kwa ajili ya mbolea ya mashambani.

Kwa kuhitimisha, madhara yatakayosababishwa na mradi huu yatakumba zaidi maeneo ya mradi pekee, na madhara yake yatakua ya muda mfupi, yanayoweza kutatuliwa kwa muda mfupi, na yanaweza kuepukika, pamoja na kwamba madhara hayo yanaweza yasijitokeze kama umakini kipindi cha utekelezaji wa mradi utapewa kipaumbele.

Katika utekelezaji wa mradi huu mbinu mbadala za kutatua chanagamoto ambazo zinaweza kujitokeza au kusababishwa na mradi ni pamoja na kuhakikisha suala la kuzuia mmomonyoko wa udogo katika eneo la mradi kipindi cha kuchimba na kufukia linazingatiwa, kuhakikisha hakuna uchafuzi wa udongo na vyanzo vya maji, kuzuia kusambaa kwa magonjwa pamoja na kuhakikisha afya na usalama wa wafanyakazi na jamii kwa ujumla.

Majibu ya utafiti huu yanaonesha kuwa, mradi huu tarajiwa utakua na manufaa makubwa kwa jamii kwani utasaidia katika kuboresha afya na usafi kwa jamii ya watu wa Mji wa Magu kwani watu watakuwa na eneo maalumu kwa ajili ya kumwaga na kutibu maji taka na kufikia kiwango ambacho hakina madhara kwa binadamu na viumbe wengine.